Kufanyika Wana

na

Ellis P. Forsman

Kufanyika Wana

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 8, 2011

Kufanyika Wana

Warumi 8:14-17

Moja kati ya njia ya urithi mkuu, huyo ya uzima wa milele, ni kufanyika wana. Wote tunapaswa kushukuru kwamba tunaweza kuhitimu kwa ajili ya utajiri wa kuurithi uzima wa milele kwa kufanyika wana. Hakuna mtu leo ambaye ana haki katika urithi, isipokuwa kwa kufanywa wana. Mtu anaweza kufanyika mwana wa Mungu kuurithi uzima wa milele.

Neno "kufanyika" haitokei kwenye Biblia mara nyingi, lakini umuhimu wake mkuu unaweza kuonekana katika uthamani na uhusiano katika urithi wa uzima na Mungu mbinguni.

Waliyofanyika kuwa wana Wakapendwa na Wakahitajika

Mtu anaweza kufanyika mwana wa Mungu kwa sababu anapendwa na anahitajika na Mungu:

Yoh. 3:16, "*Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa mwana wake wa pekee, ili kila amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*"

Mungu anatutaka sisi kama waliyofanyika kuwa wanae; na akawapenda watoto wake.

Yesu Kristo ndiye pekee mwana wa Mungu. Lakini wanawake na wanaume wa makabila yote na nchi zote, watoto wa kiume na wa kike wanawezakuwa wana wa Mungu kwakufanyika.

Mtume aliyevuviwa Paulo akaandika katika Warumi 8:14-17, "*Kwakuwa wote wanaongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu. Kwa kuwa hamkupokea tena roho ya utumwa iletayo hofu, bali mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, Aba, yaani Baba. Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, yakuwa sisi tu watoto wa Mungu; na kama tu watoto, basi tu warithi, warithi wa Mungu, warithi pamoja na Kristo; naam, tukiteswa pamoja naye ili tupate na kutukuzwa pamoja naye.*"

Kulingana na kifungu hiki, kama waliofanywa watoto wa Mungu, Wakristo wana kibali, warithi wa kiroho na Mungu, Baba, na Yesu Kristo Mwana. Uhusiano huu ni wa ajabu kiasi gani! Utarajio huu ni wa utukufu wa wakati ujao wakati ambapo maisha katika dunia hii itaharibiwa.

Kabla ya kuja kwa Kristo katika dunia, kulikuwa na agano kati ya Mungu na Israeli. Waisraeli walikuwa katika agano na Mungu, lakini wakati ungefika wa kufanyika wakati watu wote wa kila nchi, awe Myahudi au Mtaifa, waweze kufanywa wana wa Mungu.

Mtume Paulo akaandika katika Wagal. 4:3-7, *"Kadhalika na sisi tulipokuwa watoto, tulikuwa tukitumikishwa na kawaida za kwanza za dunia. Hataulipowadia utimilifu wa wakati, Mungu alimtuma mwanaye ambaye amezaliwa na mwanamke, amezaliwa chini ya sheria, ili sisi tupate kupokea hali ya kuwa wana. Na kwakuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, aliaye, Aba, yaani, Baba. Kama ni hivyo, wewe si mtumwa tena, bali u mwana, na kama u mwana, basi u mrithi wa Mungu."*

Mtume anahitimisha kwamba Israeli ilianzisha *"wana wa ahadi"*, jinsi unavyoweza kusoma katika Wagalatia 3:29 na Wagalatia 4:28. Hata ivyo, watu wote, awe Myahudi au Myunani, mwanaume au mwanamke ni wamoja katika Kristo Yesu kwa kufanyika wana wa Mungu.

Wageni Waliofanywa

Kabla ya upatanisho na kufanyika, mataifa walikuwa wageni kutoka kwa Mungu, jinsi Paulo anavyo eleza katika. Wakol. 3:21, "*Na ninyi, mliokuwa hapo kwanza mmefarikishwa, tena adui katika nia zenu, kwa matendo yenu mabaya, amewapatanisha sana."*

Lakini baada ya Kristo kuja na kuanzisha ufalme wake, kanisa lake na nafsi zili "*…okolewa…katika nguvu za giza, akatuamisha na kutuingiza katika ufalme wa mwana wa pendo lake."* (Wakol. 1:13), alafu upatanisho, ukombozi na msaha vili patikana na Mungu akawahamisha watoto wake wote katika ufalme wake. Kama watoto waliyoamishwa, wakawa warithi, *"kuurith wokovu,"* kama tunavyopata katika Waeb. 1:14.

Warithi Pamoja na Kristo

Mtume aliyevuviwa alisema moja ni "*warithi kupitia Mungu," imefunuliwa katika* Wagal. 4:7. Na "Watoto wa Mungu" wana wa Mungu, ni "warithi pamoja na Kristo," (Waru. 8:14-17). Kama *"warithi"* pamoja na Kristo, mwana wa Mungu, watoto wa Mungu wanaweza kutarajia Mungu, Baba na Kristo, Mwana kushiriki nao utajiri wote wa ufalme wa milele,kupitia umilele wote.

Neno *"Warithi"* iliyotumika katika lugha sahihi ilikuwa ni ile ya kutokurithi. Mtume Petro katika 1Pet. 3:7 ameiongelea kama mke na mume, waliyo ungana katika Kristo, kama *"kuwa warithi pamoja ya*

neema ya uzima." Mwanamke na mwanamume ambao ni wamoja katika Kristo ni watumishi wasaidizi wa Bwana na warithi wasaidizi wa utajiri wa ufalme wa milele ya Bwana.

Kama *"wraith walioungana*", pamoja na Kristo kama kaka yetu mkubwa, mmoja anahitaji haki, kipaumbele, na Baraka za familia ya Mungu. Tuwe na Baraka zipi! Ni Baraka zipi za milele tunazorithi!

Furaha iliyounganishwa na Baraka za milele Wakristo wameahaidiwa, kama warithi walioungana na Kristo, tushiriki katika utukufu wa Kristo katika umilele, kama tumeshiriki katika mateso ya Kristo duniani. Mtume aliye vuviwa Paulo anaandika:

Rumi. 8:17,*"na kama tu watoto basi tu warithi, warithi wa Mungu, warithio pamoja na Kristo, naam, tukiteswa pamoja naye ilitupate kutukuzwa pamoja naye."*

Alafu mtume Paulo akaongelea wana wa Mungu, aliposema katika Wakol. 3:3-4, *"Kwa maana mlikufa na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu. Kristo atakapofunuliwa, aliye uhai wetu ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu."*

Fikiria kuhusu hilo! Kama wewe ni mtoo wa Mungu, mrithi pamoja na Kristo, mwanaye mpendwa, lazima ujitokeze na Kristo katika utukufu. Utukufu ambao Mungu anao kwa ajili ya Mtoto wake, itashirikishwa pamoja nanyi, kama moja wa watoto wake aliyowafanya upya. Utukufu huu utakuwa wa aina gani!

Jinsi ya Kufanyika Watoto wa Mungu

Biblia inaeleza kwa uwazi hali ya kufanyika wana wa Mungu. Katika waraka wote wa Wagalatia, Paulo anaongelea kufanyika wana; jinsi walivyo fanyika wana wa Mungu, na umuhimu wa imani na ufalme kwa kufanyika wana.

Katika Wagal. 3:26-27, mtume anasema kwa kauli isiyokosewa, jinsi walivyokuwa wana wa Mungu, "*Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa nji ya imani katika Kristo Yesu. Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo."* Tafadhali angalia kwa makini matumizi ya lugha. Neno *"katika"* ni ya muhimu" *"batizwa katika Kristo," mtume alisema.*

"Maana ninyi nyote...mliobatizwa katika Kristo mmemvaa, Kristo." Ni wangapi *"waliyomvaa Kristo? "Ninyi nyote" mliobatizwa katika Kristo,"* mtume alisema. Hakika hakuna taswishi juu ya hali ya kufanyika wana wa Mungu.

Mwana wa Mungu asiye na Hatia

Mungu anapenda kwamba watoto wake wasiwe na hatia na wasijeruhiwe. Sikiliza maneno haya kutoka kwa Mungu katika 2Wakor. 6:17, *"Kwa hiyo tokeni kati yao, mkatengwe nao, asema Bwana, msiguse kitu kilicho kichafu, Nami nitawakaribisha."*

Pia katika Wafil. 2:15, "*Mpate kuwa wana wa Mungu wasio na lawama, wala udanganyifu, wasio na ila kati ya kizazi chenye ukaidi, kilichopotoka ambao kati ya hao mnaonekana kuwa kama mianga katika ulimwengu."*

Penda na Upendwe

Mzazi mwenye upendo ataweka upendo wake juu ya watoto wake wa kike na wa kiume pia, na watoto wa kiume na wa kike wenye nidhamu watapenda na kuwaheshimu baba na mama. Waef. 6: 1, *"Watoto watiini wazazi wenu katika Bwana: kwa maana hii ni haki."*

Mungu anawapenda watoto wake, na ni upendo wa jinsi gani usiyo linganishwa aliyo weka juu ya watoto wake!

Yohana, mtume wa upendo, anasema katika 1Yoh.3:1-3, "*Tazameni ni pendo la aina gani alilitupa Baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu, na ndivyotulivyo kwa sababu hii ulimwengu haututambui, kwa kuwa haukumtambua yeye. Wapenzi sasa tu wana wa Mungu, wala haujadhihirika bado utakavyo kuwa, lakini twajua yakuwa atakapodhihirishwa, tuta fanana naye, kwa maana tutamwona kama alivyo. Na kila mwenye matumaini haya katika yeye hujitakasa, kama yeye alivyo mtakatifu."*

Kupendwa na Mungu ni kumpenda Mungu na kutii mapenzi yake. Mtume anahitimisha katika:

- 1 Yoh. 4:8, *"Yeye asiyependa hakumjua Mungu, kwa maana Mungu ni pendo."*
- 1 Yoh. 4:11, *"Wapenzi ikiwa Mungu alitupenda sisi hivi, imetupasa na sisi kupendana."*
- 1 Yoh. 4:6, "*Nasi tumelifahamu pendo alilonalo Mungu kwetu sisi, na kuliamini. Mungu ni upendo, naye akaaye katika pendo, hukaa ndani ya Mungu na Mungu hukaa ndani yake."*

Huu ndiyo upendo wa Mungu kwa ajili ya watoto wake; na upendo wa wana wa Mungu kwa Baba yetu wa Mbinguni.

1 Yoh. 5:2-3, "*Katika hili twajua kwamba twawapenda watoto wa Mungu tumpendapo Mungu, na kuzishika amri zake. Kwa maana huku*

ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake, wala amri zake si nzito."

Mungu anawapenda watoto wake na watoto wake waaminifu wana mpenda. Watoto wa Mungu waliyo fanywa upya wana ahadi ya urithi mkuu ambao haujawahi kutokea kuweza kushiriki. Mungu wetu ametupatia Roho Mtakatifu kama "*arabuni"* kikomo chetu cha *"urithi wetu."*

Waef. 1:14, *"Ndiye aliye arabuni ya urithi wetu, ilikuleta ukombozi wa milki yake, kuwa sifa ya utukufu wake."*

Watoto wa Mungu waliyofanywa upya wana sehemu ya kuishi "*…tumaini katika kufufuka kwake Yesu Kristo katika Wafu, katika urithi usiyoharibika, usio na uchafu, usionyauka, uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu,"* (1 Petr. 1:3-4).

Tumaini la uzima wa Milele

Mtume aliye vuviwa Yakobo anatoa uhakika wa utajiri ambao warithi wa ufalme wataufurahia.

Anasema katika Yakobo 2:5, "*Ndugu zangu wapenzi sikilizeni, je! Mungu hakuwachagua masikini wa dunia wawe matajiri wa imani na warithi wa ufalme aliowaahidia wampendao?"*

Kutokana na maandiko haya yenye uvuvio, mambo manne ya hitimisho tunayaona:

- Mungu anawapenda watoto wake na anawapa utajiri mwingi kwa sababu ya imani na kutii kwao, hata kama ni masikini katika ulimwengu huu.
- Ndugu katika Kristo wako katika ufalme, kwa hiyo, "*warithi wa ufalme."*
- Kwa warithi wa ufalme, Mungu "*ameahidi"* Baraka za urithi wa milele. Baraka ni ahadi.
- Ahadi ya urithi imewekwa juu ya upendo: *"Kwa wale wanaompenda,"* na imani, "*matajiri wa imani."*

Isisahaulike kwamba mtume wa upendo, Yohana, anasema katika 1Yoh. 5:3, *"kwa maana huu ni upendo wa Mungu, kwamba tuzishike amri zake: na amri zake siyo ngumu."*

Kufanywa wana, Kukombolewa kwa Mwili

Mtume anasema kwa wana wa Mungu waliogeuzwa watarajie kukombolewa kwa mwili, mwili mpya, kwa ajili ya umilele.

Waru. 8:23, "*Wala si hivyo tu, ila na sisi wenyewe tulio na malimbuko ya Roho, sisi pia tunaugua katika nafsi zetu, tukikutazamia kufanya wana yaani, ukombozi wa mwili wetu."*

Miili yetu kwa ajili ya umilele haitakuwa mwili huu wa damu na nyama. Mtume amesema kuwa *"Roho"* itatoa *"uzima pia katika mwili wa kawaida,"* kama jinsi Roho alivyo mfufua Yesu kutoka katika wafu.

Warumi 8: 10-11, *"na Kristo akiwa ndani yenu, mwili wenu umekufa kwa sababu ya dhambi, bali roho yenu i hai, kwa sababu ya haki. Lakini ikiwa roho yake yeye aliye mfufua Yesu anakandani yenu, yeye alimfufua Kristo Yesu ataihuisha kwa miili yenu ilyo katika hali ya kufa, kwa Roho wake anayeka ndani yenu."*

Mtume akahitimisha swala la mwili katika uzima wa milele baada ya ufufuo katika maneno haya kutoka kwa mtume Paulo:

1 Wakor. 15:35-44, "*Lakini labda mtu atasema, wafufuliwaje wafu? Nao huja kwa mwili gani? Ewe mpumbavu! Uipandayo haihuiki, isipokuwa; nayo uipandayo, huupandi mwili, ikiwa ni ya ngano au nyingineyo; lakini Mungu huipa mwili kama apendavyo, na kila mbegu mwili wake. Nyama yote si nyama moja; ila nyingine ni ya wanadamu, nyingine ya hayawani, nyingine ndege, nyingine ya samaki. Tena kuna miili ya mbinguni na miili ya duniani, lakini fahari yake ile ya mbinguni ni mbali, na fahari yake ya duniani ni mbali. Kuna fahari moja ya jua, na fahari nyingine ya mwezi na fahari nyinge ya nyota; maana iko tofauti ya fahari hata kati ya nyota na nyota. Kadhalika na kiama ya watu hupandwa katika uharibifu; hufufuliwa katika kutokuharibika; hupandwa katika aibu, hufufuliwa katika fahari; hupandwa katika udhaifu, hufufuliwa katika nguvu, hupandwa mwili wa asili, hufufuliwa mwili war oho. Ikiwa uko mwili wa asili na waroho pia uko."*

Usiache kutoa haki

Mototo wa Mungu anataka kuhakikisha kwamba aachi haki yake ya kuurithi uzima wa milele.

Mtume Petro anasema katika 1Per. 1:3-5, *"Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa rehema zake nyingi alituzaa mara ya pili tupate tumaini lenye uzima kwa kufufuka kwake Yesu Kristo katika wafu; tupate na urithi usioharibika, usio na uchafu, usionyauka, uliotunzwa mbingunu kwa ajili yenu. Nanyi manlindwa na nguvu za*

Mungu kwa njia ya imani hata mpate wokovu uliotayari kufunuliwa wakati wa mwisho."

Lazima ikumbukwe kila mara kwamba mwana wa Mungu anaweza kuacha kuishi, muaminifu, mwana wa Mungu mtiifu. Onyo la aina hiyo inatolewa kwa watoto wa Mungu mara kwa mara tena.

- Waeb. 3:12, *"Angalieni ndugu zangu usiwe katika mmoja wenu moyo mbovu wa kutokuamini, kwa kujitenga na Mungu aliye hai."*
- 1 Tim. 4:1, "*Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani wakisikiliza roho zidanganyazo na mafundisho ya mashetani."*

Sasa sikiliza onyo hili la mwisho linalotolewa kwa wana wa Mungu katika ufalme, washiriki wa kanisa la Bwana Laodikia:

Ufu. 3:15-22, *"Nayajua matendo yako, yakuwa hu baridi wala hu moto, ingekuwa heri kama ungekuwa baridi au moto. Basi kwa sababu una uvuguvugu, wala hu baridi wala moto, nitakutapika utoke katika kinywa changu. Kwa kuwa wasema mimi ni tajiri, nimejitajirisha, wala sina haja ya kitu nawe hujui yakuwa wewe u mnyonge na mwenye mashaka na maskini na kipofu, na uchi. Nakupa shauri ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, upate kuwa tajiri na mavazi meupe upate kuvaa, aibu ya uchi wako usionekane, na dawa ya macho ya kujipaka macho yako, upate kuona, wote niwapendao mimi nawakemea, na kuwa rudi basi uwe na bidii, ukatubu. Tazama nasimama mlangoni nabisha, mtu akiisikia sauti yangu na kufungua mlango nitaingia kwake, name nitakula pamoja naye, nay eye pamoja name. Yeye ashindaye nitampa kuketi pamoja name katika kiti change cha enzi, kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi. Yeye aliye na sikio na alisikie neno hili ambalo roho inayaambia makanisa."*

Mungu hata waacha watoto wake na kuwanyima faida za urithi wa uzima wa milele. Lakini watoto wa Mungu wanaweza kumuacha Mungu, Baba wa mbinguni na kujinyima wenyewe utajiri wa urithi wa uzima wa milele mbinguni.

Bwana Mungu akatoa kanuni hii muda mrefu uliopita wakati nabii Azaria alipotaza katika 2 Nyakati. 15:2, *"naye akatoka ili amlaki Asa, akamwambia, nisikieni Ee Asa na Yuda wote na Benyamini; Bwana yu pamoja nanyi, mkiwa pamoja naye nanyi mkimtafuta, ataonekana kwenu lakini mkimwacha, atawaacha ninyi."*

Alafu mtume Petro anawatia moyo watoto wa Mungu katika 2 Petro 1:5-11 kuwa waaminifu ilikwamba asikataliwe hata mmoja kuingia katika utajiri wa ufalme:

"Naam, na kwa sababu iyo hiyo mkijitahidi sana kwa upande wenu katika imani yenu tieni na wema na katika wema wenu maarifa, na katika maarifa yenu kiasi, na katika kiasi chenu saburi, na katika saburi yenu utauwa, na katika utauwa wenu, upendano wa ndugu, upendo. Maana mambo hayo yakiwa kwenu na kujaa tele,yawafanya ninyi kuwa si wavivu wala si watu wasio na matunda, kwa kumjua Bwana wetu Yesu Kristo. Maana yeye asiye kuwa na hayo ni kipofu, hawezi kuona vitu vilivyo mbali, amesahau kule kutakaswa dhambi zake za zamani. Kwa hiyo ndugu jitahidini zaidi kufanya imara kuitwa kwenu na uteule wenu, maana mkitenda hayo hamtajikwaa kamwe. Maana hivi mtaruzukiwa kwa ukarimu kuingia katika ufalme wa milele wa Bwana wetu, mwokozi wetu Yesu Kristo."

Angalia Usianguke

Mtume Paulo aliwaonya watu wa Mungu kwa ajili ya hatari ya kuanguka.

1 Wakor. 10:12, *"Kwa hiyo anayejidhani kuwa amesimama, na angalie asianguke."*

Jinsi mtume alivyo zingati majukumu yake mwenyewe, akaandika:

1 Wakor. 9: 27, "*Bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha;isiwe, nikiisha kuwa hubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa."*

Paulo alitambua kuwa kuna uwezekano wa yeye kupotea, ataikiwa alikuwa mtume mwaminifu wa Yesu Kristo. Katika barua yake kwa Waebrania mtume aliwaonya wana wa Mungu:

Wae.3:12, *"Angalieni ndugu zangu asiwe katika mmoja wenu moyo mbovu wa kutokuamini, kwa kujitenga na Mungu aliye hai."*

Yesu aliweka wazi katika Yohana 15:5-6, *"mimi ni mzabibu, ninyi ni matawi, akaaye ndani yangu name ndani yake, huyo huzaa sana, maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote. Mtu asipokaa ndani yangu hutupwa nje kama tawi na kunyauka, watu huyakusanya na kuyatupa motoni yakateketea."*

Kristo ni mzabibu na watu wake ni matawi. Kinachotokea ni kwamba "mwanadamu" amefananishwa na "matawi" haiwezi kuendelea kukaa katika mzabibu (Kristo), na "inanyauka"? Yesu akatoa jibu: Watu "*…wakayakusanya nakuyachoma."*

Mwana wa Mungu anayepotea lazima aokolewe, amgeukie Mungu tena ili kwamba asamehewe dhambi zake (Yakobo 5:19-20). Maneno ya matamshi ya msamaha kwa motto wa Mungu aliyepotea inajumlisha:

Toba na sala, Matend.8:13-24, "*Na yeye Simoni mwenyewe aliamini akabatizwa, akashikamana na Filipo, akashangaa alipoziona ishara na*

miujiza mikubwa inayotendeka. Na mitume waliyokuwako Yerusalemu, waliposikia yakwamba Samaria imelikubali neno la Mungu, wakawapelekea Petro na Yohana, ambao waliposhuka wakawaombea wampokee Roho Mtakatifu; kwa maana hajawashukia hata mmoja wao ila wamebatizwa tu kwa jina lake Bwana Yesu. Ndipo wakaweka mikono yao ju yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu. Hata Simon alipoona ya kuwa watu wanapewa Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono ya mitume, akataka kuwapa fedha akisema, nipeni na mimi uwezo huu ili kila mtu nitakayemweka mikono yangu, apokee Roho Mtakatifu. Lakini Petro akamwambia, Fedha yako na ipotelee mbali pamoja nawe, kwa kuwa umedhania karama ya Mungu inapatikana kwa mali. Huna fungu wala huna sehemu katika jambo hili, kwa kuwa moyo wako si mnyofu mbele za Mungu, basi tubia uovu wako huu, ukamwombe Bwana ili kama yamkini usamehewe fikira hii ya moyo wako. Kwa maana nakuona u katika uchungu kama nyongo, na tena u katika kifungo cha uovu. Simoni akajibu, akasema, Niombeeni ninyi kwa Bwana yasinifikilie mambo haya mliosema hata moja."

Kukiri dhambi. Yakobo 5:16, "*Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii."*

Labda haiwezi kurithiwa

Baba mzuri anawapenda watoto wake na kuwapa mahitaji. Baba mzuri anaye wapenda watoto wake anawafanyia maandalizi kwa mapenzi yake, kwa faida yao baada ya kufa kwake. Hataivyo, inawezeka baba asiwarithishe watoto wake.

Baba yetu wa mbinguni anawapenda watoto wake na amewapa utajiri wa maisha. Mungu hata waacha watoto wake, lakini wanaweza wakamuacha, hivyo wakashindwa kupata urithi wao.

Mungu Hashindwi

Baba yetu wa mbinguni anawapenda watoto wake na ame *"watunzia mbinguni" urithi usio haribika, na hachafuki,na kwamba haiyeyuki, imetunzwa mbinguni kwa ajili yako,"* (1 Petr. 1:4)

1 Wakor. 2:9, *"Lakini kama ilivyoandikwa,mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia (wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu,) mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao."*

Upendo wa Mungu hauwaangushi watoto wake. Watoto wake nao lazima wasimuangushe.